JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO
Ithibati ya Ubora Kimataifa (ISO 9001:2015)

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na.** KA.57/173/01A/5 **06 Novemba, 2025**

Makatibu Wakuu Wote,
Makatibu Tawala wa Mikoa wote,
Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama,
Wakurugenzi Wakuu wa Mashirika ya Umma wote,
Wakuu wa Idara Zinazojitegemea Wote,
Watendaji Wakuu wa Mamlaka/Wakala za Serikali Wote,
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Majiji, Miji, Manispaa na Wilaya Zote,
**TANZANIA BARA.**

**Yah: MWALIKO WA KUSHIRIKI KIKAO KAZI CHA SITA (06) CHA MWAKA CHA SERIKALI MTANDAO TAREHE 10 – 12 FEBRUARI, 2026 AICC ARUSHA**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

2. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ina jukumu la Kuratibu, Kusimamia, Kuendeleza na Kukuza jitihada za Serikali Mtandao, pamoja na kuhimiza uzingatiwaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma.

3. Katika utekelezaji wa jitihada hizo, Mamlaka imeandaa Kikao Kazi cha Sita (06) cha Serikali Mtandao, kitakachofanyika tarehe **10 - 12 Februari, 2026** katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha - **AICC jijini Arusha**. Aidha, tarehe **09 Februari, 2026** itakuwa ni siku maalum kwa ajili ya usajili wa washiriki, hivyo washiriki wote watatakiwa kufika na kujisajili kwa tarehe husika.

4. Kikao Kazi hiki kitawakutanisha takriban Wadau 1200 wa Serikali Mtandao kutoka katika Tasisi na Mashirika ya umma, ili kujadili jitihada za Serikali Mtandao, Changamoto na namna ya kuzikabili. Mgeni Rasmi katika kikao hiki ni **Katibu Mkuu Kiongozi.**

5. Kikao hiki kitaongozwa na kaulimbiu isemayo *"**Kuboresha Utendaji wa Serikali kwa Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Umma Kupitia Mifumo Salama na Jumuishi ya Serikali Mtandao" - (Transforming government operations by enhancing public service delivery through integrated and secure government solutions).***

6. Kwa barua hii, ninawaalika **Maafisa Masuuli (Accounting Officers)**, **Wakurugenzi/Wakuu wa Idara na Vitengo vya TEHAMA**, **Maafisa TEHAMA na Watumiaji wote wa mifumo ya TEHAMA (Maafisa Ununuzi na Ugavi, Mawasiliano Serikalini, Mipango, Wahasibu, Rasilimali Watu, Watunza kumbukumbu n.k**.) kuhudhuria na kushiriki Kikao hicho.

7. Aidha, kila mshiriki atapaswa kulipa ada ya ushiriki **Tsh. 800,000/=** kupitia mfumo wa TSMS **(www.tsms.ega.go.tz),** ili kupata namba ya malipo na kisha kulipia. Washiriki watapaswa kulipa mapema kabla ya mfumo kufungwa tarehe **31 Januari, 2026** saa **11.00 jioni.**

8. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia dawati la Msaada wa kiufundi kwa baruapepe **egov.helpdesk@ega.go.tz** au kwa simu namba **0764292299 Au 0763292299**.

Nashukuru kwa ushirikiano wako.

Digitally Signed By
BENEDICT BENNY NDOMBA
Thu Nov 06 18:12:34 EAT 2025

BENEDICT BENNY NDOMBA

**MKURUGENZI MKUU**

**Nakala:** Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais,
IKULU,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
**40400 DODOMA.**